


Harith Swaleh

Chaguo La Wanavyuoni

Yaliyomo

1. **Shukrani na Heshima**
   Makumbusho .... a – b

2. **Sehemu ya Kwanza**
   Dibaji .... 1 – 10

3. **Tarekhe za Tabiin** .... 11 – 31

4. **Sehemu ya Pili**
   Utangulizi .... 32 - 33

5. **Tarekhe za wanavyuoni wa Afrika Mashariki** .... 33 – 65

6. **Vitabu vilivyotumika** 65

Heshima na Makumbusho

Kwa unyenyekevu mkubwa na kwa moyo wangu wote nakitoa tunu kitabu hiki kwa:

1) Hujjah Al-Islam Abu Haamid Al-Ghazali (Died 1111A.D)

2) Muhyiddin Abu Zakariyya Al-Imam Al-Nawawi (Died 1277A.D)

Sehemu ya Pili

UTANGULIZI

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu (s.w.t). Nadua pamoja na amani zimfikie Mtume wetu Muhammad (s.a.a.w.a.w.s), pamoja na Aal na Masahaba (r.a.a).

Mara nyingi watu wa aina mbali mbali wameonesha imani yao kwangu kwamba nitaweza kuwaandikia kitabu juu la wanavyuoni wa Mashariki ya Afrika. Hakika hili ni jambo zuri, kwani watu kuwa na imani na wewe, ni kuheshimu ujuzi wako na kuwa na imani kwamba ujuzi huo utatumiwa kwa namna unaofaa.

Ndani ya miaka ishirini iliyopita nimetoa hotuba nyingi za kuhusiana na wanavyuoni au mwanchuoni wa Mashariki ya Afrika, na mara nyingi nimekuwa na majadiliano pamoja na watu wanaofanya utafiti na uchunguzi juu la mwanachuoni maalum.

Ama ndani ya miaka mitano iliyopita maombi ya kuandika kitabu cha aina hiyo yamekuwa mengi zaidi kutokana na watu mbali mbali.

Kuhusu umuhimu na ugumu wa uandishi kama huu ni kitu ambacho kiko wazi kabisa, na hakina haja ya kujadiliwa.

Pamoja na hivyo, kitabu hiki, ingawa ndani yake wamo wengi katika wanavyuoni wa Mashariki ya Afrika, nimeona ni jambo muhimu kuwa na mkufu ambao pana maungano kati yao na mababu zao wa mbali katika ulimwengu wa kiislamu.

Kwa hivyo, nakariri na nazidi kuweka wazi kwamba wanavyuoni wa Mashariki ya Afrika wametajwa katika kitabu hiki na wameunganishwa pamoja na wanavyuoni wengine walioko katika miji ambayo inazingatiwa kwamba ni mashina na vitovu vya Uislamu.

Sababu ya kuchukuwa msimamo kama huu, ni kwamba wako wanavyuoni walio tangulia ambao wamekwisha kauandika juu la wanavyuoni wa Mashariki ya Afrika na vitabu vyao vimewahi kutumika na kumalizika na baadaye kupatikana toleo jipya likiwa kama sahihisho.

Chukua mfano, Shaykh Abdalla Swaleh Farsy, kitabu chake "wanavyuoni wa Mashariki ya Afrika", ni kitabu kilichotolewa zamani na kikatumika zamani, na napenda kusema, tangu 1970 mpaka sasa ni taabu kupata nakala hiyo ya asili, licha ya kwamba utapata kitabu hicho katika maduka yetu.

Kweli, kitabu hiki baadaye kimefasiriwa kwa kiingereza na Dkt. Randall Lee Powels, lakini tatizo ni kwamba kitabu hiki chapatikana Amerika na wanao kipata mara nyingi ni wasomi, weingi wao wakiwa ni wa nchi za kigeni.

Liko na toleo la Kiswahili peke yake, lakini tatizo ni kwamba, kimechapishwa Uingereza na wengi walio bahatika kupata nakala hiyo huku Mashariki ya Afrika ilikuwa ni kwa ghafla au kitu kama zawadi.

Ajabu kubwa ni kwamba toleo la Dkt. Pouwels ni la mwaka 1989, watu wengi hapa Mashariki ya Afrika kamwe hawajui habari hizo, na wakijua pana ugumu mkubwa wa kukipata kitabu hiko.

Kwa hivyo kitabu juu la historia ya wanavyuoni wa Mashariki ya Afrika kiko, na kiemadikwa vizuri na mwandishi wa kitabu hicho, Shaykh ABdalla Swaleh Al-Farsy, aliyekuwa Chief Kadhi hapa Kenya (aliyestaafu) Mwenyeezi Mungu amrehemu na amlipe mema.

Katika hiki chetu, lengo kubwa ni kwamba wako wanavyuoni ambao hawakupata bahati ya kutajwa majina yao katika kitabu cha Shaykh Abdalla, bila ya yeye kukusudia kufanya hivyo, au kwamba ingekuwa ni furaha yake kukosekana majina ya watu watukufu kama hao.

Sababu ya pili, siku zilizopita nilikuwa nikifahamu kwamba tatizo letu ni kuwajuwa wanavyuoni wa Mashariki ya Afrika. Lakini ukweli wa mambo

ni kwamba upungufu huu uko katika kutowajuwa wanavyuoni wa kutoka mahali mbali mbali na nyakati mbali mbali, katika ulimwengu.

Nikizidi kuyaweka wazi maneno haya, wengi wana wajuwa kina Imam shafi, Imam Abu Hanifa, Imam Ahmad, Imam Malik, lakini, pamoja na hivyo, liko tatizo katika ujuzi huu. Na hii si kwa ajili kwamba hawana uwezo wa kufahamu, lakini tatizo liko katika upande huu: vitabu vya kueleza mambo hayo ni nadra kupatikanwa katika masoko ya Mashariki ya Afrika, na walio bahatika kuvipata na kuvisoma vitabu kama hivi walikosa bahati ya kusomesha mambo kama haya, kwani mara nyingi vitabu kama hivyo huwa haziko katika ratiba ya kusomesha msikitini au madrasa illa kwa wanafunzi wa kiwango cha juu kabisa.

Sitofurahi kabisa ikiwa mtu yeyote atafahamu kwamba mambo haya yalikuwa hayajulikani, lakini ukweli ni kwamba hayakupata bahati ya kujulikana na wengi kama inavyotakikana

Kwa hivyo utakuta pana ugumu mkubwa sana kwa wengi, wa kutofautisha kati ya baadhi ya Maswahaba na baadhi ya tabiina wa mstari wa mbele, na vile vile kupambanua wazi wazi tabiina wa mwanzo na waliokuja katika vipindi vya mwisho.

Tatizo la aina hii pia liko katika kutofautisha bain ya wanavyuoni wakubwa. Nikitowa mfano aweza mtu kutoona taabu pindi unapo mwambia kwamba al-Imam Ahmad alikuwa akifurahi sana alipokuwa akikutana na mwanfunzi wake Ibn Qudama, lakini alikuwa akifurahi zaidi wakati akitembelewa na mwanafunzi wake halisi Ibn Rajab.

Hivi ni kusema Imam Ahmad hakuwa aweza kabisa kukutana na Ibn Qudama wala Ibn Rajab.

Mfano mwengine: Safari moha Imam Shafi alikuwa akistaajabu sana kwa uhodari wa mwanafunzi wake Al-Imam Al-Bukhari, lakini alifurahi mno na akaomba Mungu sana juu ya mwanafunzi wake Imam Nawawi alipoandika kitabu chake ambacho ni sherehe ya Swahih Muslim.

Imam Shafi alipokufa umri wa Imam Al Bukhari ulikua ni miaka minane na ilikua hapana namna ya Imam Shafi na Imam Nawawi kukutana.

Nasema tena wanavyuoni wetu watukufu walio tutangulia sisi walikuwa ni mahodari sana wa mambo hayo, lakini uhodari huu ulikosa bahati ya kuendelezwa mbele, kwa kutosomeshwa masomo kama haya, pamoja na uhaba wa vitabu vyake.

Kwa sababu hizi nilizozitaja, kitabu hiki ni chaguo langu juu la wanvyuoni wetu watukufu.

Ni matarajio yangu, pia kusudio langu, kwamba watu wa viwango mbali mbali vya elimu na tabaka mbali mbali za ufahamu watanufaika kwa uandishi huu, na wale walio mabingwa hapana shaka watazidi kufanya bidii kusomesha na kueneza elimu na maarifa kama haya.

Namuomba Mwenyeezi Mungu (S.W.T.) atutimizie lengo hili tukufu na atakase kusudio na nia ya mwandishi iwe tu ni kwa ajili yake yeye (S.W.T.) na atie baraka zake. Amin.

HARITH SWALEH
16/11/03

Na sasa tungependa tuanze na wanavyuoni wa:-

BARAWA

Katika wanavyuoni wa kibarawa ni:-

1) Shaykh Muhyiddin Bin Shaykh Bin Abdalla Al-Qalitany Al-Waily (1724 – 1869 A.D)

Huyu ni mmoja wa wanavyuoni wakubwa wa Ukanda wa Pwani

wa Afrika ya Mashariki. Alizaliwa Barawa mwaka wa 1794 AD na akafa 1869AD.

Alizaliwa huko Barawa na akasomeshwa na wanavyuoni wa Kisomali, kisha akaenda mji wa Lamu ambapo alibaki kwa mda mrefu huku akinufaika kutoka kwa wanavyuoni wa hapo kama kina Shaykh Muhammad wa Inyekai Mkuu, {Muhmmad Bin Abubakar Bin Muhammad (1140AH – 1220 AH)} (Inyekai Abubakar).

Baadaye alikwenda Mombasa ambapo alishiriki katika vita baina ya Mazrui na Sayyid Said, kwa kutunga mashairi ya kuwaunga mkono kina Mazrui. Lakini baada ya siku chache alibadilisha msimamo na akawa pamoja na kina Ma-Albusaidy.

Aliwahi kuwa kadhi katika mahakama ya Sayyid Said na ya Sayyid Majid.

Aliwahi kuandika vitabu kwa kiarabu kama fafanuzi juu la utangulizi wa kitabu cha Imam Nawawy: Minhaj Al-Talibin, pia kitabu katika Elimu ya Tawheed (Elimu ya tabia na sifa za Mwenyeezi Mungu); kadhalika Elimu ya Sarf (Arabic Morphology). Baadhi ya vitabu aliviandika kwa lugha ya Kiswahili kama: Utenzi wa Miraji, na swala ya kuombea mvua.

Shaykh Muhiddin aliwacha baadhi ya wanafunzi waliokuwa mahodari sana kama:-
Sheikh Abdul-Aziz Abdula Ghani wa kutoka Barawa, Sheikh Muhammad Bin Ahmad Al-Moroni, Sheikh Fadhil Bin Ali Mbagwa na Shaykh Hagan Bin Yusuf (wote watatu kutoka Ungazija). Na wanafunzi wengine ni Sayyid Ahmad Bin Salim na Abubakar Bin Salim.

Katika mambo muhimu Shaykh Muhyiddin aliyatimiza, ni kwamba alienda Makka kuhiji ambapo alikutana na wanavyuoni wakubwa

wa Kiislamu kutoka pembe mbali mbali.

2) Shaykh Abdul-Aziz Abdul-Ghani Al-Amawy (1834 – 1896)

Huyu alikuwa ni mwanafunzi wa Shaykh Muhyiddin na alikuwa ni mwanafunzi wa mwanachuoni wa kutoka Hijaz, kwa jina la Shaykh Ahmad al-Maghriby.

Shaykh Abdul-Aziz, alizaliwa Barawa na akasoma huko Barawa hasa elimu ya Tasawwuf (Elimu ya kujikaribisha, kumfikiri na kumcha Mwenyeezi Mungu (S.W.T.). Katika mwaka wa 1848, shaykh wake, shaykh Muhyiddin aliashiria yeye awe Kadhi wa Kilwa. Na baadaye alikua Kadhi wa Zanzibar katika utawala wa Sayyid Barghash.

Pia yeye alikuwa rafiki msiri wa Sayyid Khalifa na Sayyid Ali (watoto wa Sayyid Said).

Shaykh Abdul-Aziz alikuwa akihitilafiana na wanavyuoni wa ukanda wa pwani katika mbinu zake za kuutumikia na kuufundisha Uislamu kwa sababu alikuwa akiendelza na kuusambaza mpango wa Dhikri, Tariqa Qadiriyya. Tariqa za dhikri wakati huo hazikueko pwani ya Kenya.

Zaidi ya yote haya, Shaykh Abdul-Aziz alikuwa ni katika mashaykh walio simama imara kupinga mashambulio ya wazungu kama waingereza na wajerumani.

Mtoto wa Shaykh Abdul-Aziz alikuwa ni Shaykh Burhani Bin Abdul-Aziz, mtu ambaye alikuwa ni katika Mashaykh wa Zanzibar na akawahi kuwa kadhi mkuu chini ya utawala wa Mwengereza. Na baadaye, cheo hicho kilishilikwa na Sayyid Umar Bin Sayyid Ahmad Bin Sumeyt.

Hapa kulipatikana wanavyuoni wakubwa kama Shaykhul-Islam, Mwenye Abudi; Shaykh Kale Bin Mbwarahaji, Shaykh Siraj Fakihi Aweso, Shaykh Lali Vae, na wengineo. Ilimu yao, baada ya kuchunguzwa na wanavyuoni ilionekana yatoka pahali pa tatu; napo ni:-

Kutoka kwa wanavyuoni wa:-

i) huku huku kwetu
ii) kutoka kwa wanavyuoni wa Kisomali
iii) kutoka kwa Shaykh Faqihi Aweso mwanachuoni aliyesoma mpaka Iraq, kisha akaja kuishi kwenye visiwa hivi, na akazaa mtoto aliemuita Siraj Fakihi Aweso. Shaykh Faqihi alikufa 1270 AH.

1) MWENYE ABUDI (1844 – 1922)

Jina lake kamili ni Sayyid Abdulrahman Bin Sayyid Ahmad As-Saggaf – Shaykhul-Islam.

Alizaliwa Siyu na akapata masomo yake hapo Siyu kwa wanavyuoni wa Kisomali na Kibajuni.

Alianza kupokea masomo ya kidini kutoka kwa mwanachuoni wa Lamu, Sayyid Abubakar bin Abdulrahman al-Husayny (Mwenye Manswab).
Kisha baadaye akasoma elimu za Fiqh, Nahw na Swarf kutoka kwa Shaykh Ali bin Umar (Msomali) na akasoma tafsiri na hadithi kutoka kwa Shaykh Faqih Uways (faqih Aveso) (Msomali) na akasoma Fiqh zaidi kutoka kwa Shaykh Lali Vae (Mbajuni).

Shaykh Fakihi Uways jina lake ni Shaykh Umar. Mtoto wake ni Shaykh Abdulkarim bin Shaykh Umar bin Muhammad bin Mahmud aliekufa mwaka 1858. Shaykh Zubair bin Ali Al-Barawi ambae alisoma Chundwa kwa Shaykh Umar Stambul akamaliza masomo

yake huko Madina Al-Munawwara na baadae akarudi Chundwa. Kaburi yake ni karibu ya msikiti wa Muhdhar. Katika wenzake ni Shaykh Kale bin Mbwarahaji, Shaykh Waly bin Abubakar Al-Hatimy, huyu alikua kigogo, alie hamia Unguja akasomesha huko na akafa huko.

Shaykh – Islam kwanza alikuwa Kadhi wa Siyu na baadaye utawala wa Muingereza ulimchagua awe Kadhi Mkuu wa Ukanda wa Pwani.

Shaykh –Islam amewacha wanafunzi wengi mashuhuri sana. Miongoni mwao ni:-

i) Shaykh Abdul-Majid bin Zahran (Shaykh Abudi), alikua kadhi wa Lamu, na akafa mwaka wa 1364 AH, na akazikwa Lamu.
ii) Shaykh Said bin Ahmed wa Lindi (Tanzania)
iii) Shaykh Abdalla al-Husni – (Mombasa) amezikwa, nje ya mskiti anisa

Katika watu waliosoma na Mwenye Abudi ni Sheikh Kale bin Mbwarahaji bin Bwana Mkuu, aliyekufa mwaka wa 1320 AH na Sheikh Siraj Faqih Aveso aliyekufa mwaka wa 1316 AH.

Mwenye Abudi na Shaikh Kale walisoma Rasini kwa Mwenye Umar Bin Hashim, hasa ilimu ya Fiqhi na Tafsiri.

Katika wanafunzi wake Shaikh Kale ni:-

i) Shaykh Muhammad Abshir (aliyekufa 1961)
ii) Shaykh Salil bin Ahmad (aliyekufa 1966)
Na wengineo.

Shaykh Shauri bin Haji Mshirazi (aliyekufa mwaka wa 1913 A.D.)

Alizaliwa Donge, Pemba. Alisoma kwa Shaykh Muhyiddin bin Shaykh Al-Qahtany Alwaily. Alipokea fani mbali mbali za masomo ya Uislamu na lugha ya Kiarabu. Alikuwa hodari zaidi katika fani ya Tafsiri. Shaykh Shauri aliacha wanafunzi wawili:-

i) Shaykh Hajj bin Vuai Mshirazi aliekufa mwaka wa 1937 A.D.
ii) Shaykh Ali bin Umar Mshirazi aliyekufa mwaka wa 1925.

Shaykh Sheshe bin Seko (aliekufa mwaka wa 1909 A.D.)

Alipokea masomo yake kwa Shaykh Ali bin Abdalla Mazrui.

Shaykh Sheshe alibarikiwa kwa maisha marefu na kufaulu kwa daraja kubwa kuufundisha na kuutangaza Uislamu katika mji wa Tanga.

Shaykh Said bin Ahmad Mkilindi.

Alisoma kwa Shaykh Ali bin Abdalla na alikuwa Kadhi wa Takaungu.

Shaykh Abdalla Bakathir hapo Unguja

Shaykh Abdalla bin Muhammad bin Salim Bakathir alizaliwa Lamu Mkomani mwaka 1860. Baba yake alikufa akiwa na umri wa miaka minne. Katika kuinukia kwake alikua huku akisoma na wakati huo huo akishona kofia kwa cherehani. Katika mashekhe wote wa Lamu ni Sayyid Abubakar bin Abdurrahman (Mwenye Manswabu) na Shaykh Abubakar bin Shaykh Muhammad bin Shaykh Abubakar (Bwenye Kai) na Habib Swaleh bin Alwy Jamalil-Leil.

Tangu mwaka wa 1892, Shaykh Abdalla Bakathir alianzisha daraza zake mpaka mwaka wa 1902. na kuanzia mwaka wa 1902, shaykh Abdalla alinunua nyumba katika mtaa wa "Ukutani" huko Unguja. Kulikuwepo na msikiti katika mtaa huu. Tangu wakati huo, kusomesha kulikuwa ni katika sebule ya nyumba hiyo mpaka kufa kwake mwaka wa 1925 A.D Alikuwa akisaidiwa kusomesha na wanafunzi wake wawili waliokuwa wakiishi pamoja naye. Nao ni:-

i) Shaykh Muhsin bin Ali al-Barwany na
ii) Shaykh Muhammad bin Umar al-Khatib.

Baada ya Shaykh wao kufa, waliendesha darasa hii ya Ukutani na shamba "Kitundu" kama alivyokuwa akifanya Shaykh wao wakati wa uhai wake.

Darasa hii ya Ukutani kwa vile ilivyokuwa mashuhuri ilifanywa iwe ni "Maahadi ya Ukutani (Ukutani Institute) na serikali ya Muingereza.

Na katika wanafunzi mashuhuri wa Shaykh Abdalla Bakathir ni Sayyid Umar bin Sayyid Ahmad bin Sumayt, na mtoto wake Shaykh Abubakar bin Shaykh Abdallah, Shaykh Muhsin bin Aly Al-Barwani, Shaykh Habib Umar Aly Al-Mazrui na Habib Umar bin Sumait.

Kila akitaka kumtaja Shaykh Abdalla alikuwa ni lazima asema hivi: - Amesema Shaykh Abdalla;" "Alikuwa Shaykh wetu Abdalla."

Shaykh Abubakar bin Shaykh Muhammad (Bwenye Kai) (aliekufa mwaka wa 1891)

Alipokea masomo yake kwa:-

i) Mzazi wake Shaykh Muhammad bin Shaykh Abubakar (Inyekai Mkuu)
ii) Shaykh Muhammad bin Fadhil al-Bakry aliesoma Madina kiasi cha miaka 33 kisha akarudi Lamu na akawasomesha

kina Bwenye Kai. Shaykh Muhammad bin Fadhil alikufa

iii) Sayyid Abdulrahman bin Ahmed al-Husainy katika ukoo wa Shaykh Abubakar bin Salim aliekufa 1856.

Katika wanafunzi wa Bwenyekai ni:-

a) Ndugu yake Shaykh Ali bin Muhammad al-Maawy aliekufa mwaka 1930.

b) Shaykh Faisal bin Ali bin Abdalla al-Laamy. Shaykh Faisal kisha alienda kusoma Madina kwa miaka 22. (Alikufa 1918).

c) Sayyid Abdalla bin Ahmad al-ahdaly (Mwenye Abdalla Kadhi). Huyu pia ni mwanafunzi wa Shaykh Faisal. Mwenye Abdalla Kadhi alisoma kwa

Bwenyekai wakati mmoja na Sayyid Swaleh bin Alwy Jamalilleyl. Vile vile Mwenye Abdalla Kadhi alikuwa Kadhi wa Lamu baada ya Shaykh Muhammad bin Ali bin Msellem al-Amiry – aliyekuwa hodari sana katika elimu za Nahw, Swarf na Fiqh.

d) Shaykh Ali bin Khalid al-Lamy.

<u>Shaykh Ali bin Khalid al-Laamy na shaykh Abdalla bin Shaykh Muhammad bin Umar al-Khatib al Maawy.</u>

Wanavyuoni hawa wawili ni katika wale waliofanya kazi kubwa sana Nairobi
hasa mitaa ya Pumwani na Pangani.

Shaykh Abdalla kazi yake ilianza Lamu kasha akafanya kazi Unguja na baadaye akaenda Nairobi pahali ambapo alimalizia Umri wake. Ililazimika arudishwe Lamu baada ya kuzeeka sana na kutokea harakati za Mau Maumwaka wa 1953 na akafa hapo Lamu 1954.

Shaykh Abdalla ni katika wale mashaykh wachache wa Africa ya Mashariki ambao walizuru Hadhramaut akiwa pamoja mwanachuno mashuhuri,

Sayyid Ahmad bin AbiBakr bin Sumayt.

Na Shaykh Ali bin Khalid, baada ya kusoma kwao lamu na kufanya kazi huko, alikwenda Nairobi na akatumia wakati wake mwingi sana kufundisha na kuongoza. Lakini katika miaka ya mwisho ya umri wake alifanya kazi Mombasa na akawasomesha watu wengi, miongoni mwao wakiwa ni Shaykh Muhammad bin Ahmad bin ali al-Bereky al-Laamy, na vile vile mwanafunzi wa Shaykh Bereki – Shaykh Ali Seneda (Shaykh Gunda).

Katika maisha yake ya Mombasa alifundisha misikiti mbali mbali, lakini alitangaa zaidi kwa kusomesha katika msikiti Musa hapo majengo. Alikufa Mombasa 1944.

Sayyid Abu Bakar bin Abdulrahaman al-Husainy (Mwenye Manswab)

Huyu ni katika wanavyuoni walioishi maisha marefu. (Kulingana na Profesa Idha Salim (1973), aliishi miaka 94, yaani 1828 – 1922 A.D. Na kulingana na Shaykh Bahsan (1989) aliishi miaka 97, yaani 1243 – 1340 A.H)

Mwenye Manswab ni Shaykh wa Mashyakh wengi mashuhuri, kama vile:-

i) Habbib Swaleh bin Alwy Jamalilley (1844 – 1935 A.D.)
ii) Shaykh Abdalla bin Muhammad Bakathir
iii) Shaykh Abdalla bin Muhammad al-Khatib.
iv) Sayyid Ahmad Badawy bin Sayyid Swaleh Jamalilley I.

Mashaykh wake hapa Lamu ni:-

a) Shaykh Muhammad bin Fadhil al-Bakry – Huyu ndiye Shaykh wake mkubwa aliyekufa 1283 A.H.
b) Sayyid Abdulrahman bin Sayyid Ahmad bin Abdulrahman al-Husainy aliekufa mwaka 1272 A.H.

Ama huko Makka alisoma kwa:-
Sayyid Ahmad bin Zayni Dahlan na Hadhramaut akasoma kwa Sayyid Aidarus bin Umar al-Habshy.

Mabongo ya Afrika Mashariki hapo Makka:-

1) Shaykh Ali bin Abdalla Mazrui
Alisoma kwa Shaykh Ahmad bin Muhammad ad-Dimyaty aliewahi kuwa mufti wa Makka

2) Sayyid Abu Bakr bin Abdulrahman (Mwenye Manswab)
Alisoma kwa Sayyid Ahmaed bin Zayni Dahlan.

3) Sayyid Ahmad bin Abubakar bin Sumeyt.
Alisoma kwa Sayyid Muhammad bin Husain al-Habshy, na wengineo.

4) Shaykh Abdalla bin Muhammad bin Salim Bakathir – Alisoma kwa Shaykh Umar bin Abu Bakar Bajunayd na Shaykh Muhammad bin Said Babsayl. Shaykh Babsayl Aliwahi kuwa mufti wa Makka.

5) Shaykh Abu Bakar bin Shaykh Muhammad (Bwenye kai) ama Shaykh huyu alifika Makka wakati wa msimu wa Hijja. Alikaribishwa kuendesha darasa na mwanachuoni mkubwa kwa jina la Sayyid Abu Bakar bin Sayyid Muhammad Shatwaa ad-Dimyaty, mwenye vitabu mashuhuri katika Afrika ya Mashariki kama:-

i) Ad-Durar al-Bahiyya.
ii) Hashiyat Iaana at-Talibin.
iii) Hashiyat ad-Dimyatiy alal-Waraqat.

Bwenye kai alikuwa mashuhuri hapo Makka kwa ajili ya wanafunzi wake wengi waliokwenda kusomea zaidi huko makka.

6) Mbali na hawa, kuna wale mashaykh walio kaa Makka mpaka wakaitwa kina Mwenye wa Makka nao ni:-

i) Mwenye wa Makka Mdogo – Sayyid Abu Bakar bin Sayyid Alawy Ash-Sahtiry (aliekufa 1340 A.H.)
ii) Mwenye wa Makkar Mkubwa – Sayyid Abdulrahman bin Abi Bakr al-Hamidy (aliekufa 1301 A.H)

Hawa ni watu waliotoka lamu wakakaa miaka mingi Makka mpaka wakastahiki kupata majina kama hayo.

Maana ya Mwenye wa Makka, ni Sharifu wa Makka.

Shaykh Ali bin Abdalla bin Nafii al-Mazrui

Alizaliwa 1825 na akafariki 1894. Huyu ndiye babake Shaykh Al-amin bin Ali al-Mazrui.

Babu yake, Shaykh Nafii, alikuwa ni katika wanavyuoni wakubwa wa Kiibadhi. Na babake Shaykh Ali, Shaykh Abdalla, pia mwamzo alikuwa ni miongoni mwa wanavyuoni wakubwa wa Kiibadhi.

Katika mwaka wa 1837, Shaykh Ali na babake walisafiri wakenda Makka na wabakia huko wakisoma kwa wanvyuoni wakubwa wakubwa mpaka mwaka wa 1846. Shaykh Abdalla hakurudi tena Mombasa kwani alibaki Hadhramaut akizidi kusoma kwa wanavyuoni wa huko mpaka akafariki Shihri mwaka wa 1846.

Shaykh Ali alirudi Mombasa na akafanya kazi kubwa Zanzibar na Mombasa ya kuwalingania watu mbali mbali kati yao wakiwa Ma Ibadhi, ili wawe Masunni wa dhehebu la Imam Shafii.

Shaykh Ali aliwahi kufanya kazi akiwa kadhi wa Mombasa chini ya utawala wa Sayyid Majid (1836 – 1870).Baadaye alirudi tena Makka ili kupanuwa

masomo yake katika mwaka 1859.

Safari hizi za Shaykh Ali za kimasomo ziliwanufaisha sana watu wa Mombasa na wa Unguja. Hii ilikuwa ni sababu kubwa ya kuusimamia na kuutangaza Uislamu na Usunni. Jambo hili lakini lilimfanya Shaykh Ali kupata taabu upande wa serikali hasa katika utawala wa Sayyid Majid katika mwaka wa 1887, Shaykh ali alifungwa jela na Sayyid Barghash. Aliachiliwa mwaka ulio fuatia.

Baada ya hapo, Shaykh Ali zaidi alishughulika na kusomesha na kupambana na mambo mbali mbali ambayo alikuwa akiyaona hayalingani na mafundisho ya Uislami halisi.

Katika wanafunzi mashuhuri wa Shaykh Ali ni Shaykh Suleiman bin Ali Mazrui ambaye alikuwa ni kadhi wa Mombasa 1910, na akawa Chief Kadhi 1932. Hakuwahi kumsomesha mgtoto wake kwa sababu alipofariki, shaykh Al-amin alikuwa ni mtoto wa miaka minne.

Shaykh Al-Amin bin Ali al-Mazrui (1891 A.D. – 1947 A.D)

Jina lake: Shaykh al-amin bin Shaykh Ali bin Shaykh Abdalla bin Shaykh Nafii al-Mazrui.

Shaykh huyu ni katika watu ambao wenye misingi ya kiibadhi, kwani babu yake Shaykh Nafii alikuwa ni katika wakuu wa wanavyuoni wa Kiibadhi.

Baba yake, Shaykh Ali bin Shaykh Abdalla alikufa akiwa yeye (Shaykh al-Amin) ni mtoto wa miaka minne. Kwa hivyo hakuwahi kusoma kwa babake. Lakini, shaykh wake halisi ni Shaykh Sulaiman bin Ali Al-Mazrui ambaye alikuwa ni mwanafunzi wa Shaykh ali (yaani Shaykh Ali alikuwa ndiye Shaykh wake mkuu). Pia Shaykh Sulaiman alikuwa ni mkwe wa Shaykh al-Amin.

Na baadaye alisoma sana kwa shaykh Abdalla bin Muhammad bin Salim

Bakathir, na kwa Sayyid Ahmad bin Abu Bakar bin sumeyt. Na katika watu wa kutoka miji mikubwa ya Kiislamu walio acha athari kubwa kwa shaykh al-Amin ni:-

i) Shaykh Jamalu-ddin al-Afghani.
ii) Shaykh Muhammad Abduh.
iii) Sayyid Muhammad Rashid Ridha.

Sahykh al-amin ndiye aliyekuwa akimuongoza na kumshauri mwanfunzi wake shaykh Ghazali kuiendesha Madrasatul Ghazali iliyofunguliwa 1933 A.D.

Shaykh Al-Amin aliandika vitabu vingi vya Kiswahili juu ya makadiani, Ukristo, Urathi katika Uislamu, Tafsiri ya Juzuu Amma, na msururu wa vitabu vilivyo itwa Muongozo. Pia aliandika kwa kiarabu vitabu kama Hidayatul Atfali, al-Ahadithul Mukhtarah. Pia alikuwa akitoa gazeti lililo itwa al-Islah. Shaykh Al-Amin alisafiri sana katika mashariki ya Afrika na akatenda mengi.

Wanafunzi Mashuhuri wa Shaykh al-Amin bin Ali Mazrui

1) Shaykh Muhammad Qassim Mazrui (1912 – 1982)

Shaykh al-Amin alikuwa ni mwalimu wake, mjombake na mkwe wake.

Baada ya masomo yake, shaykh Muhammad alianza kazi ya uwalimu, na akawa kadhi mwaka 1946. Aliwahi kuwa kadhi wa Mombasa, Lamu na Malindi.

Mwaka wa 1963 alipandishwa daraja akawa kadhi mkuu mpaka mwak 1968 alipostaafu. Cheo hiki alikitumikia kwa mda wa miaka mingi kabla ya 1963; kwani pale Sayyid Ali Badawy alipoacha kazi ya kadhi mkuu, Kenya alikuwa haina kadhi mkuu.

Shaykh Muhammad alikuwa ni mwalimu hodari, mwandishi bora na kadhi mwadilifu. Kitabu chake, "Historia ya Utumwa katika Uislamu na nyengine" ni ushahidi wa kutosha juu la ubingwa wake.

Vilel vile Shaykh Muhammad Qassim alisoma kwa Shaykh Sulaiman bin Ali bin Khamis al-Mazrui ambaye ni mwalimu na mkwe wa Shaykh al-Amin bin Ali.

2) **Shaykh Rashid bin Qassim (1915 – 1952)**

Huyu ni nduguye Shaykh Muhammad Qassim. Hawa ndugu wawili walishirikiana kufanya mengine mazuri kuhusu Uislamu.

3) **Shaykh Muhammad bin Ahmed bin Ali (Shaykh Bereki).**

4) **Shaykh Ali bin Hemed al-Buhry.**

5) **Shaykh Abdalla Swaleh Farsy.**

6) **Maalim Said bin Ahmad.**

Sayyid Ahmad bin Abu Bakar bin Abdalla bin Sumayt

Huyu ni Sharifu wa kihadhrami. Babake ni mzaliwa wa Shibban, Hadhramaut na (babake) alikuwa na maarifa mazuri ya masomo ya kidini na unahodha wa majahazi. Pia aliwahi kuwa kadhi wa Zanzibar katika utawala wa Sayyid Majid.

Na Sayyid Ahmad pia alikuwa na vipawa kama hivyo vya babake, lakini babake alimwamrisha awache unahodha na aendelee na masomo ya dini. Kwa hivyo kwanza alisoma kwa babake huko Ungazija (Grand Comoro); ambaye alikuwa amestaafu baada ya kufa Sayyid Majid. Kisha akasoma kwa Sayyid Abul Hassan bin Ahmad Jamalillayl. Baadaye alienda Zanzi-

bar akasoma kwa mwanachuoni wa Iraq, kwa jina la Sayyid Abdul Hussein bin Ali al-Mar'ashy ambaye alikuwa amefanya makao yake hapo Unguja katika mwaka 1886 A.D.

Kati ya 1883 – 1886, alifanywa Kadhi, pamoja na hivyo alifanya safari mara tatu za kwenda Hadhramaut kupanuwa masomo yake, mara ya mwisho ikiwa ni 1907 A.D.

Pia alisafiri kwa muda wa miaka mitatu kwenda katika miji mikubwa ya Kiislamu. Katika mwaka 1886, alikwenda Istanbul (Uturuki), ambapo alikaa kiasi cha mwaka mmoja huku akisoma kwa Sayyid Fadhil Basha bin Alwy bin Sahl, kitu ambacho kilimpa umashuhuri mpaka akawa ni mtu wa mstari wa mbele wa Khalifa Abdul Hamid (Khalifa wa Uturuki wa wakati huo). Khalif huyu alivutiwa sana na Sayyid Ahmad mpaka akamtuza mojawapo katika nishani za dola ya Uturuki.

Baadaye katika mwaka 1887, alihudhuria katika chuo kikuu cha Kiislamu Misri (Al-Azhar); kisha akaenda Makka kwa lengo hilo hilo la masomo.

Ilikua kukipotokea tofauti kati ya wanavyuoni wawili wa Zanzibar, watu hawa walikuwa wakimpelekea da'wah (Kesi) yao mwanachuoni mkuu wa Makka, Shaykh Muhammad Said bin Muhammad Babseyl, wakitaka kupata ufafanuzi wake ju ya kadhia hiyo.

Majibu ya Shaykh Babseyl yalikuwa ni kama ifuatavyo:-

> "Kwa nini hamupeleki da'wa (Kesi) hii kwa Sayyid Ahmed bin Abu Bakar bin Sumayt? Kwani sisi tumepata umashuhuri kuliko yeye kwa sababu ya kuishi huku Makka"

Wanafunzi wake:-

Miongoni mwa wanafunzi wake mashuhuri ni:-

i) Habib Umar bin Ahmad bin Sumayt.

Huyu alikuwa ni mtoto wake na ni mwanafunzi wake. Naye alipata bahati kama ile walioipata wazee wake. Kwa hivyo alifanya kazi kubwa na kushikilia vyeo mbali mbali baada ya kufa babake.

Mr. Justice Reed, aliyekuwa hakimu hapo Zanzibar wakati huo aliungana kwa kusema haya:-

> "Sayyid Umar bin Sumayt hakuwa ni mwanachuoni wa kuheshimika hapa Zanzibar tu lakini alikuwa ni mtu mashuhuri, anayetambuliwa vile vile katika nchi za mbali kama Misri na kwingineko."

Sayyid Aidarus bin Sayyid Swaleh Jamalilleyl (1305 – 1388 A.H.)

Huyu ndiye aliye endeleza maendeleo ya msikiti wa Riadha (Lamu), baada ya kufa Sayyid Ahmad Badawy. Riadha ni msikiti na chuo muhimu sana katika Afrika ya Mashariki kuhusiana na masomo ya Elimu za Kiislamu na lugha ya kiarabu (pamoja na elimu zake).

Aliweza kuunganisha na kustawisha amendeleo haya kwa kuishi pamoja na kushirikiana na watoto wa Sayyid Ahmad Badawy waliozaliwa na mama mbali mbali, hasa mtoto wa kwanza wa huyu Sayyid Ali, ambaye ni Sayyid Muhammad Bahsan bin Sayyid Ali (ambaye wakati huo huo ni mjukuu wake yeye Sayyid Aidarus – akiwa ni baba wa mamake).

Walimu wa Sayyid Aidarus: Alianza kusoma kwa Sayyid Ali bin Sayyid Abdalla (ambaye ni ami yake Habib Swaleh); kisha akasoma kwa:-

ii) Baba yake (Habib Swaleh)

iii) Sayyid Abdalla bin Sayyid Ahmad al-Ahdaly.

iv) Sayyid Abu Bakar bin Sayyid Alwy Shatry (Mwenye wa Makka)

v) Shaykh Faisal bin Ali bin Abdalla Allamy.

Sayyid Aidarus alikuwa na uhusiano mzuri na babake. Na alikuwa akimsaidia katika mambo mengi yanayo ambatana na safari. Baada ya babake kuzeeka, alikuwa akitumia wakati mwingi pamoja naye; na alikuwa ndiye mkaribishaji wa wageni wa babake.

Alizaliwa mwaka mmoja na ndugu yake Sayyid Ahmad Badawy, (ambaye alimtangulia kwa miezi sita).

Sayyid Ahmad Badawy bin Sayyid Swaleh Jamalileyl(Mwenye Badawy) 1305-1358 A.H)

Walimu wake:

i) Sayyid Swaleh
ii) Sayyid Ali bin Sayyid Abdalla (Mwenye Sayyid Ali)
iii) Sayyid Abubakar bin Sayyid Abdulrahman (Mwenye Maswab) na huyu ndiye shaykh wake mkubwa (shaykhu Fat-hi-hi)
iv) Sayyid Abdalla bin Sayyid Ahmad al – Ahdaly (Mwenye Abdalla Kadhi)
v) Shaykh Faisal bin Abdalla al – Laamy
vi) Shaykh Ali bin Muhammad al –Maawy.
vii) Shaykh Abdalla bin Muhammad Bakathir ambaye pia ni mkwe wake (Babu yao kina sayyid Ali Badawy)

Sayyid Ahmad ndiye aliyekuwa akisomesha, kusilihisha na kufanikisha hafla za aina mbali mbali.

Yeye ndiye aliye anzisha mfumo wa Madrasa ambapo watoto watakaa kwenye mabao,wasomeshwe fani mbali mbali,wafanyiwe mitihani na ilikuwa ni baada ya watoto hawa kuhitimu Qur'an ndio wapelekwe madrasa. Alipokufa, aliwacha pengo kubwa sana ambalo lilikaribia kuleta mpasuko wa aina maalum.kulipatikana suluhisho kupitia kwa juhudi za wanavyuoni wakubwa wa lamu kama Sayyid muhammed bin Sayyid Abdalla Ar-Rudainy, Shaykh Muhammad bin Shaykh Ali bin shaykh Muhammad al- Maawy, Shaykh Muhammad bin Maawiya bin Muhammad pamoja na wazee wa mji wa Lamu pia kazi hii iliweza kufaulu kwa vizuri

sana kupitia kwa msaada wa aina maalum wa Habib Umar bin Sumayt wa unguja na Shaykh al- Amin bin Ali al-Mazrui wa Mombasa pamoja na mabwana watukufu wa mji wa Mambrui.

Wakati alipokufa Sayyid Ahmad Badawy mji wa Lamu, vitongoji vyake na Afrika ya Mashariki yote zilitingishika kabisa, na Lamu haikurudi katika cheo chake iliokua nacho pmaka hivi leo.

Katika walioathirika sana ni:
1) Shaykh Muhammad bin Ali Al-Maawy
2) Sharif Said bin Sayyid Abdallah Al-Biidh
3) Shaykh Abdalla bin Umar Al-Khatib
4) Shaykh Abdulmajid bin Zahran
5) Shaykh Al-Amin bin Ali Al-Mazrui
6) Habib Umar bin Habib Ahmad bin Sumayt

Sayyid Ali bin Sayyid Ahmad Badawy (1325-1407 AH)

Huyu ndiye mtoto wa kwanza wa Sayyid Ahmad Badawy .Kwanza kabisa alisoma kwa babu yake mkubwa Sayyid Ali bin Sayyid Abdallah, na ndiye aliyempa jina hili.

Kisha akasoma kwa babu yake Habib Swaleh, kisha kwa babake Sayyid Ahmad Badawy, baadaye akawa wakati mwingi anasoma kwa Shaykh Muhammad bin Ali al-Maaway, ambaye ndiye shaykh wake mkubwa (shaykh fat-hi-hi) wakati huo huo akawa anasoma kwa wanavyuoni mbali mbali kama Shaykh Abdalla bin Muhammad Khatib, Sayyid Muhammad bin Abdalla Ar-Rudainy.Shaykg Abdalla bin Ali al-Maawy, na Shaykh Abdulmajid bin Zahran.

Upande wa Zanzibar alisoma kwa babu yake Shaykh Abdalla bin Muhammad Bakathir (kwa mda mfupi) kwa mjombake Shaykh Abu Bakr bin Shaykh Abdalla Bakathir, kwa Sayyid Ahmad bin Abu Bakr bin Sumayt na kwa Sayyid Umar bin Sayyid Ahmad bin Sumayt.Na mombasa alisoma

kwa Shaykh Ali bin Khalid, na zaidi kwa Shaykh al- Amin bin Ali al-Mazrui.

Ma shaykh wake walipendezwa sana na yeye kwa sababu alikuwa hodari sana hasa kwenye masomo magumu zaidi kama mirathi, elimu za kujua nyakati za swala (miqat), Elimu za kujua undani na utamu wa lugha za kiarabu (Nahw, Swarf, Balagha)

Na katika Fiqh, Sayyid Muhammad bin Abdalla Rudainy, Shaykh Abdul Majid bin Zahran na Habib Umar bin Sumayt walikuwa wakiona kama kwamba Sayyid Ali ameumbiwa ilimu hii. Na hivyo hivyo ndivyo waliyokuwa wakionelea kina Shaykh al-Amin bin Ali katika Elimu za Miqat na Hadith.

Ama Shaykh wake mkubwa, Shaykh Muhammad bin Ali alikuwa akimuona uhodari wake katika ilimu zote alizosomesha. Kuna kitabu kiitwacho "Majmu ul Matun", kikiwa na maana "kitabu kilichokusanya ilimu mbali mbali za kiislamu na kiarabu". Basi Shaykh Muhammad bin Ali alikuwa akisema,

"Katika uhodari wa Sayyid Ali Badawy ni kwamba aweza kusomesha ilimu zote hizi kwa uhodari mkubwa".

Shaykh Muhammad bin Ali alikuwa ni rafiki wa babake Sayyid Ali, na mwanafunzi wa babu yake (ambaye ni Habib Swaleh). Kwa hivyo Shaykh Muhammad kwa hawa watu watatu alikuwa ni <u>mwalimu rafiki, ndugu rafiki</u> na <u>mwanafunzi rafiki</u>.

<u>Habib Swaleh bin Alwy Jamalil-Layl (1844-1935)</u>

Al-Imam, Al-Mujahid, Al-Mujaddid, Al-Mujtahid. Huyu ndie muanzilishi wa msikiti wa Riyadha, ambao ulikuwa ni msikiti na ni Kulliyyah (College).

Wanafunzi walimiminika kwenda kusoma Riyadha kutoka sehemu mbali mbali za Afrika ya Mashariki.

Nitafurahi kama nitamakinika kuandika kitabu kizima juu la Habib Swaleh.

Sayyid Muhammad Bin Abdalla Ar-Rudainy (aliyekufa 1381 A.H)

Walimu wake

i) Shaykh Faisal bin Ali bin Abdallah Al-Lamy (huyu ndie Shekhe wake mkuu)
ii) Shaykh Ali bin khalid
iii) Shaykh Ali bin Muhammad bin Shaykh Abubakar al-Maawy, ambaye alisomesha elimu ya tafsiri na Figh.

Katika wanafunzi wake mashuhuri:
i) Sayyid Ahmad Badawy
ii) Shaykh Muhammad bin Ali Al-Maawy
iii) Sayyid bin Sayyid Adnaan Al-Ahdaly
iv) Sayyid Aly bin Sayyid Ahmad Badawy
v) Sayyid Muhammad bin Twalib bin Sayyid Abdallah Al-Rudayny. Huyu alisoma sana kwa ami yake.

Sayyid Muhammad bin Adnan al-Ahdaly(1896 – 1963)

Waalimu wake:-

i) Sayyid Abu Bakar bin Abdulrahman (Mwenye Manswab)
i) Sayyid Abu Bakar bin Abdulrahamn Ash-Shatiry (Mwenye wa Makka)
ii) Shaykh Ali bin Muhammad al-Maawy.
iii) Sayyid Muhammad bin Abdalla Ar-Rudainy.
iv) Shaykh Ali bin Khalid al-Laamy.
v) Shaykh Faisal bin Ali al-Laamy
vi) Sayyid Abdalla bin Sayyid Ahmad al-Ahdaly – Huyu ni ami yake, mkwewe na Shaykh wake mkubwa (Shaykh Fat-hi-hi).

Kwa hivyo, Sayyid Muhammad Adnan alikuwa amevutiwa sana na Sayyid Ahmad Badawy, Athari hii ilibaki kwake mpaka alipo aga dunia. Na wengine ambao athari zao zilikuwa kubwa zaidi katika maisha yake yote ni:-

i. Abu Hamid Muhammad bin Muhammad al-Ghazaly (1058-1111 A.D.)
ii. Sayyid Abdalla bin Alwy al-Haddad (1044 – 1132 A.D.)
iii. Sayyid Ali bin Sayyid Abdallah Jamal-Lilyl (1844-1922).

Wanafunzi wake:-

1. Shaykh Muhammad bin Abdalla bin Masu'd
2. Shaykh Ali bin Shaykh Muhammad bin Ali al-Maawy.
3. Shaykh Ali bin Abdalla bin Muhammad al-Jahadhmy (Shaykh Aly wa Bwana Abdallah Boke)
4. Shaykh Athman bin Abu-Bakar bin Muhammad al-Laamy.
5. Shaykh Muhammad bin Abdalla bin Umar al-Khatib.
6. Bw. Muhammad bin Hilal bin Abdalla bin Faraj al-Mafaazy.
7. Bw. Ali bin Hassan Mshangama.
8. Bw. Ali Salim Basaida.
9. Sayyid Ahmed bin Sayyid Muhammad al-Husainy (Badawy wa Mwenye wa Nana)
10. Sayyid Abdalla bin Sayyid Abu-Bakar bin Sayyid Abdalla al-Hussainy (Shee Abdalla wa Shee Bakari).
11. Mwandishi wa kitabu hiki ambaye anamzingatia Shaykh huyu pamoja na Shaykh Muhammad bin Ali al-Maawy kuwa ndio Mashaykh wake wakubwa zaidi.
12. Sayyid Ahmad na Sayyid Ali (ambao ni watoto wake) japokuwa Shaykh wao mkubwa ni shaykh Salim bin Jumaan.
13. Sayyid Ahmad bin Manswab (Sayyid Abdalla bin Sayyid Alwy bin Ahmad al-Ahdaly).
14. Shaykh Muhammad bin Ali pamoja na nduguye Shaykh Ahmad bin Ali bin Abdulrahman bin Umar al-Khatib.

15. Shaykh Ahmad pamoja na ndugu zake Dkt. Abdalla na Shaykh Abu Bakar bin Muhammad bin Abubakar al-Khatib.
16. Maalim Mbarak bin Twahir.
17. Maalim Amir Awadh
18. Shaykh Ahmad pamoja na ndugu yake Faraj bin AbuBakar al-Jahadhmy ambao Sayyid Muhammad alikuwa amemuoa shangazi yao. Kwa hivyo aliwaleya.
19. Shaykh Muawiya bin Abdurrahman bin Muawiya.
20. Sayyid Abdurrahman bin Sayyid Ahmad Badawy. (Mw. Khitamy)
21. Sayyid Alwy bin Sayyid Ahmad Badawy. (Mzee Mwenye)
22. Sayyid Muhammad Bahsan bin Sayyid Ali bin Sayyid Ahmad Badawy.
23. Shaykh Hemed bin Swaleh bin Hemed Al-Bu-saidi (Shaibu Hemedi)

Shaykh Abu Bakar bin Shaykh Abdalla Bakathir (1881-1943)

Huyu ni mtoto wa pili wa Shaykh Abdalla na ni mwanafunzi wake ambae amesoma vitabu vingi kutoka kwa babake. Katika mwaka 1925, baada ya kufa babake alikwenda Makka na akabaki huko kiasi cha miezi sita akizidi kusoma kwa ma shaykh mbali mbali. Ama Hadhramawt, alienda pamoja na babake na wakavuna mema sawa kwa sawa. Shaykh Abdur-Rahman al-Mash-hur alikuwa akipendezwa sana na Shaykh Abu Bakar. Alikuwa ni hodari sana katika kutafsiri Qu'rani na kutoa mawaidha.

Shaykh Ahmad bin Muhammad Mlomry

Alizaliwa yamkini mwaka 1873 na kufariki 1936, Kwanza alisoma kwa Shaykh Ahmed bin Muhammad al-Murony, na Shaykh Abdur-Rahman Mbamba na Mashaykh wengine wa Unguja.Mwaka wa 1888, alikwenda Mombasa akasoma
kwa Shaykh Ali bin Abdalla al-mazrui mpaka 1894 Shaykh Ali alipokufa. Alibaki Mombasa akisoma kwa Shaykh Muhammad bin Qassim al-Maamiry

mpaka kufa kwake mwaka 1910. Shaykh Mlomry alisafiri sana kwa ajili ya kutafuta elimu. Alikwenda mpaka Makka, Sham (Syria) na misri, huko Misri alikutana na mwanachuoni mkubwa, Al-Imam Shaykh Muhammad Abduh (1849-1905). Na Makka alikutana na Shaykh Muhammad bin Sulayman Hasballah, mwandishi wa kitabu: Ar-riyadh al-Badiah. Shaykh Mlomry alikuwa akisomesha kwenye msikiti Baraza, Unguja. Katika wanafunzi wake mashhuri ni Shaykh Abdallah Swaleh Farsy.

Shaykh Muhammad bin Ahmad bin Ali Bereki, Al-Lamy (1910-1986)

Alizaliwa mwaka 1910 Lamu na akafariki Mombasa 1986.

Waalimu wake:

i) Shaykh Abdalla bin Muhammad al-Khatib, na huyu ndiye Shaykh wake mkubwa.
ii) Sayyid Ahmad Badawy – huyu ndiye aliempa shauri la kwenda kusomesha Vanga; na badaye Mombasa.
iii) Sayyid Abdalla bin Sayyid Ahmad al-Ahdaly,
iv) Shaykh Abdul Majid bin Zahran.

Mwaka 1934, Shaykh alikwenda Mombasa kwa muda mfupi. Kisha akaenda Vanga, na huko ndipo alipoanza kumsomesha Shaykh Ali Seneda (Shayklh Ali Gunda). Baadaye alikwenda Mombasa kwa mara ya pili, ambapo alikuwa akisomesha Msikiti wa Shaykh Mbaruku. Mahali hapa palibahatika sana, kwani Wanafunzi wengi walimaliza masomo yao hapo. Kisha akasomesha msikiti wa Azhar hapo Baghani, mpaka kufa kwake.

Shaykh Bereki katika maisha yake ya Mombasa alisoma kwa Shaykh al-Amin bin Ali Mazrui (hii ikiwa ni amri ya Shaykh wake Sayyid Ahmad Badawy) na kwa Shaykh Ali bin Khalid hapo mskiti wa Musa, na nyumbani kwake (yeye Shaykh Ali bin Khalid).

Wanafunzi wake mashuhuri

Wanafuzi wa Shaykh Bereki ni wengi. Mashuhuri katika wao ni;

i) Shaykh Ali Seneda (Ali Gunda)
ii) Shaykh Nassor Muhammad Nahdy (aliye kuwa kadhi mkuu Kenya)
iii) Shaykh Abdulrahman Muhammad Hatimi
iv) Shaykh Goso bin Ibrahim (aliyekuwa kadhi)
v) Shaykh Ali Muhammad Mwinzagu (kadhi wa mombasa)
vi) AbulHassan Sayyid Muhammad bin Sayyid Hassan (mwenye karama ambaye ndiye anaye somesha darasa zote za Shaykh Bereki hapa Masjid Azhar Baghani)

Shaykh Ali bin Hemed al-Buhry

Alizaliwa Tanga, alikuwa kadhi kutoka 1921 mpaka 1935.Alikufa 1957

Waalimu wake;

i) Shaykh Hemed al Buhry (Baba yake mzazi)
ii) Shaykh Khamis bin Salim
iii) Shaykh Abdalla Saadiq Bawazir
iv) Shaykh Hemed bin Juma al Buhry
v) Shaykh Amir Juma al-Bimani

Maalim Said bin Ahmad

Alizaliwa 1915. Alisoma kwa Shaykh al-Amin na Shaykh Abdalla al-Husni, na kwa Sayyid Ali Badawy. Tangu 1937, alikuwa ni khatib na Imam wa swala ya Ijumaa. Mwaka 1945, alianza kwenda gerezani (jela) kuwapa wafungwa mawaidha. 1952 alianza kutowa wadhi kupitia sauti ya Mvita, baadaye sauti ya wilaya ya Pwani, na kasha sauti ya Kenya.Katika uwanja wa kulingania, kuutangaza na kuueneza Uislamu, sidhani kwamba yuko aliyemfikia yeye katika hirimu zake. Shaykh huyu (Maalim Said bin Ahmad) aliendelea kutoa mawaidha sehemu mbali mbali za Kenya, misikitini na

ıabarabarani kama Mwẹmbe Tayari.

;ayyid Muhammad Bahsan bin Sayyid Ali Badawy (1344-399 A.H)

Íuyu ni mtoto wa kwanza wa Sayyid Ali bin Sayyid Ahmad Badawy. Áama yake ni binti wa Sayyid Aidarus bin Sayyid Swaleh Jamalileyl.

Vaalimu wake;

i) Sayyid Ali bin Sayyid Ahmad Badawy
ii) Shaykh Muhammed bin Ali al-Maawy
iii) Sayyid Muhammad bin Adnan al-Ahday.

ıada ya Habib Swaleh na watoto wake, Sayyid Ahmad Badawy na Sàyyid idarus, Sayyid Muhammad ni wa daraja ya nne katika kuitumikia, kufanya dii na juhudi kwa ajili ya Riyadha. Wanafunzi wake Mashariki ya frika,hasa Kenya na Tanzania ni wengi. Katika wao ni Ustadh Swaleh n Muhammad Bahsan bin Sayyid Ali Badawy (Shaykh Buhsani), Sharif luhsin bin Sayyid Ali Badawy.

haykh Abdalla Waziri Msujini (Alikufa Unguja 1904)

ikuwa ni mmoja katika wanavyuoni wakubwa wa Unguja na wakili wa po pia. Wakati wa utawala wa Sayyid Ali bin Said nyota ilipanda na awa kama mufti na waziri wa mambo ya pesa na Waqf. Shaykh Abdalla ı Waziri anatajika sana mpaka leo kwa umahiri (ustadi) wake wa kufasiri ıra'n kwa lugha ya Kiswahili, hata Shaykh Abdush-shakur, ambaye kuwa mwingi wa kuchambua wanavyuoni wenziwe alikuwa akiungama ramba tafsiri ya Shaykh Abdalla Waziri ni tafsiri bora.

ıaykh Muhammad bin Shaykh Abdalla Wazir, Msujuni

ıyu alishikilia cheo cha baba yake cha kusomesha na kufasiri Qur'ani

katika msikiti wa Chale. Ubingwa wake wa tafsiri ulizidi hata ule wa babake. Watu wengi wa Unguja walikuwa wakihudhuria darasa zake za tafsiri kuliko darasa za mwanachuoni mwengine yeyote. Wakili wa Ki-Punjabi, kwa jina la Sayyid Muhammad Hassan alitaka kuutumia ubingwa wake wa kutafsiri Qur'an, kwa hivyo alimueka Shaykh Muhammad nyumbani kwake na akawa anamlipa Rupia 50 kila mwezi huku akisaidiwa na karani mahsusi wa kumcharazia (kumpigia taipu) ili apate kutoa tafsiri ya Qura'n iliyo andikwa kwa lugha ya kiswahili.

Aliwahi kufasiri juzuu 28 kati ya juzuu 30.Lakini wanavyuoni wa Unguja walipo jua kwamba Sayyid Muhammad Hassan amenuia kupigisha chapa hiyo tafsiri walikataa na kupinga vikali huku wakitoa vipengele vyao. Hapo Sayyid Muhammad Hassan alimuachisha kazi Shaykh Muhammad na baadaye akachukuwa zile juzuu 28 akaenda nazo bara Hindi (India)

Shaykh Muhammad alisoma kwa baba yake mzazi na kwa Sayyid Ahmad bin Abi Bakr bin Sumayt, ambaye alikuwa ni mwanafunzi wa babake Shaykh Abdalla Wazir. Shaykh Muhammad alikufa mwaka 1963 akiwa na umri wa miaka 60.

Shaykh Hassan bin Umayr Shirazi

Alizaliwa huko shamba, Makunduchi mwaka 1883, na akalelewa na kukulia mjini. Mwaka 1909, yeye alikuwa ni mwalimu wa kufundisha Qurani katika shule ya Serikali.Yeye alifundisha Muyuni Makunduchi na hapo kiembe samaki. Baadaye alienda kufundisha chake chake, Pemba, ambapo alikutana na mwanachuoni wa Ki-Ibadhi, Shaykh Abdalla bin Amur al –Azry.Alisoma kwa Shaykh huyu mpaka akawa hodari katika fani mbali mbali za elimu.

Mwaka 1945, aliacha kazi ya kusomesha akawa karani wa kotini. Na mwaka huu huu alikutana na Sayyid Ahmad bin Sumeyt na mwanachuoni wa Ki-Ibadhi, Shaykh Ali bin Muhammad Mandhry, wanavyuoni ambao walimsomesha na kuzidi kumkunjua katika ujuzi wake.

Waalimu wake wengine ni;

i) Shaykh Abdur-Rahman bin Hamud
ii) Shaykh Muhammad bin Shaykh Abdalla Waziri.
iii) Shaykh Said bin Muhammad bin Dahman

Shaykh Hassan alisomesha sana Unguja nyumbani kwake Msufini, na katika Msikiti Mwembe Tanga. Baada ya hapo alihamia Tanganyika na akafundisha dini huko mpaka 1959 ambapo serikali ili shurutisha arudi Unguja. Yalipotokea mapinduzi ya Unguja mwisho wa Shaaban, 1964, mara moja alipewa cheo cha Kadhi Mkuu, Unguja na Pemba. Shaykh Hassan ameandika vitabu vingi kwa lugha ya kiarabu kama;
"Madarij al-ulaa, Sharh Tabaraka Dhil-Ulaa"na ameandika tafsiri ya Qurani kamili juzuu 30, ambayo bado kupigishwa chapa, sijui kwa nini!

Mashekhe wa Malindi na Takaungu

1) Shaykh Sulayman bin Ali bin Khamis al-Mazrui.
Alizaliwa Takaungu, alisoma kwa Shaykh Ali bin Abdalla al-Mazrui ambaye ni jamaa yake na ni mkwe wake. Alikuwa ni kadhi wa Takaungu tangu 1895 hadi kufa kwake 1910.

2) Shaykh Nassor bin Ahmad bin Muhammad al-Mazrui.
Alizaliwa Takaungu, akasoma huko na Mombasa kwa Shaykh Ali bin Abdalla al-Mazrui. Aliwahi kuwa kadhi wa Takaungu, kisha Malindi kutoka 1906, akaendelea mpaka 1946. Alikufa na umri wa miaka 80. Alijenga msikiti unao julikana kwa jina la "Msikiti wa Shaykh Nassor"

3) Shaykh Khalfan bin Abdalla al-Mazrui.
Alizaliwa 1886 Takaungu na akaanza kusoma huko kisha akaenda Mombasa akasoma kwa Shaykh Ali bin Abdalla al-Mazrui. Alikuwa kadhi wa Takaungu na jirani ya Takaungu, tangu 1918 mpaka 1925. Alikufa 1944 akiwa na miaka 78.

4) Hajj Shaykh bin Faqih bin Shaykh.
   Huyu ni mmoja wapo katika wanavyuoni wa Malindi. Katika kazi zake ni kwamba alitia maelezo katika vitabu "Witriya" katika kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W.W.) na "At-tayyib al-Asma" katika kumuomba Mwenyezi Mungu kwa majina yake matukufu (S.W.T)

Shaykh Abdalla bin Swaleh bin Abdalla bin Swaleh Al-farsy

Alizaliwa mtaa wa Malindi, Jongeani, Unguja mwaka 1912.Alipokuwa mdogo, hapo nyumbani alijulikana kwa jina la "Bwanamkubwa", wakikusudia "Wewe ni babu yetu Bwana Abdalla."

Mwaka 1924 alipelekwa shule inayojulikana hivi sasa kwa jina la Forodhani Girls School, Unguja.Mwaka 1925 aliacha shule hii na akajiunga na shule inayoitwa Mnazi mmoja Primary School ambayo sasa yajulikana kwa jina la Ben Bella Girls School.Mwaka 1930 mpaka 1932, alijiunga na shule ya kufundisha Ualimu.Shaykh Abdalla alijifundisha kusoma Qura'ni kutoka kwa mwanamke wa Kingazija, Bibi Zawadi (Fatma) binti Hamad bin Saidi (1854-1936), mpaka akahitimu na baadaye akahifadhi.

Alijifundisha Tajweed, kuandika kwa hati za kiarabu na maarifa ya kwanza ya lugha ya kiarabu kutoka kwa Shaykh Abdul-Barri Al-Jyzy kutoka kwa mwaka 1924-1929. Shaykh huyu wa Ki-Misri alileletwa na Serikali ya Unguja. Alishikilia kazi ya kufundisha Shule, akawa mwalimu, kisha Mwalimu Mkuu kisha Mkaguzi tangu mwaka 1933 mpaka 1960. Mwaka 1960 mpaka 1967, alikuwa kadhi wa Unguja. Na tangu mwaka 1968, alipewa cheti cha U-Kenya na akatunukiwa cheo cha kadhi Mkuu wa Kenya.

Mashekhe wake;

i) Sayyid Hamid Manswab
   Inaaminika kwamba huyu ndiye Shaykh aliyesomesha

kitabu kidogo muhimu kiitwacho Ar-risalah al-Jaamiah ambacho kilikuwa ufunguo mwema kwa Shaykh Abdalla. Huu ulikuwa ni mwaka 1925.

ii) Sayyid Alawy Abdul-Wahab
Alisoma kwake vitabu vidogo mashuhuri.

iii) Shaykh Ahmad bin Muhammad Mlomry Huyu ndiye Shaykh wake mkubwa (Shaykh Fathi-hi). Alisomesha fani mbali mbali ambazo mwanachuoni yambidi azijue.

iv) Shaykh AbuBakr bin Shaykh Abdalla Bakathir.Alipokea kwa Shaykh huyu Tafsiri ya Qura'ni Tukufu kwa bidii kubwa, naye Shaykh Abu Bakr akawa anamtia hima kwa kuhudhuria katika darasa zake za Ramadhani na nyinginezo. Pia katika mwaka 1930 alimpa Uimamu wa swala ya Taraweih na baada yake akampa Uimamu wa witr katika msikiti Gofu.

iv) Shaykh Muhammad bin Abdulrahman al-Makhzumy. Alisoma sana kwake vitabu vya Fiqh kama: Iqnai, Fath al-Muin, na Minhaj, na hii Minhaj alisoma mwaka 1936. Ama elimu ya kujua nyakati za swala na kutoa Qibla (Ilm al-Meeqat) alisoma kwake mwaka 1944.

v) Sayyid Umar bin Sayyid Ahmad bin Sumeyt
Alisoma kwake elimu ya Mantiq (Logic) na vitabu vingi vya fiqh.

vi) Shaykh Muhsin bin Ali al-Barwany al-Harithy.
Alihudhuria sana darasa zake mbali mbali hapo msikiti Gofu, na vile vile alikuwa akienda kusoma kwake katika nyakati mahsusi. Yeye ndiye Shaykh wake wa mwanzo aliyempa ruhusa kutafsiri Qur'ani hapo msikiti Baraza katika mwezi wa Ramadhani mwaka 1944. Shaykh

Muhsini huyu ndiye babake Shaykh Ali bin Muhsin, mwenye kitabu Tarjama ya "Al-Muntakhab" katika Tafsiri ya Qur'ani Tukufu. (1995)

Katika mwaka 1950, Shaykh Abdalla Swaleh alipigisha chapa tafsiri ya baadhi ya sura za Qura'ni, nazo ni Yasin, Waqiah, mulku, na Kahf.Na kabla ya hapo Shaykh Abdalla alikuwa akifasiri Qur'an katika Msikiti Baraza kila Alkhamisi na Ijumaa, pamoja na mwezi mzima wa Ramadhani, tangu mwaka 1944 hadi 1967, wakati alipohamia Mombasa,Kenya.

Tafsiri kamili ya Qur'an Takatifu ya Shaykh Abdalla ilichapishwa na Islamic Foundation, Qura'n House, Nairobi mwaka 1969.

TRS

Vyuo vilivyoandikwa na mwandishi huyu

Nyota ya Haki (1964)

Utangulizi wa Tafsiri ya Qur'an (1984)

Hadithi za Mtume Muhammad zilizochaguliwa kutoka Riyadhul - Swalihin (Tafsiri ya Kiswahili) 1988

Sunnah na Utukufu wake (1992)

Uungu na umoja Wake (1993)

Mwanamke na cheo chake (1994)

Ugimbi, madawa ya kulevya na madhara yake (2001)

Designed and printed by **Bajaber Printing Press**
Tel: 0722 665374 / 0733 568797 / 0720 318288 / 0735 568948
Email: osmanmarjan@yahoo.com